

SHULE YA SEKONDARI ROCHE,
S.L.P. 437,
TARIME.
SIMU: 0787109645 Au 0713509405.
12/12/2020

KUMB.NO.ROSS/AD F.1/VOL.1/2021.

JINA LA MWANAFUNZI.....

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI ROCHE, WILAYA YA RORYA, MKOA WA MARA KWA MWAKA 2020.

1.0.UTANGULIZI

Ninafurahi kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza (I)-2021 katika shule hii ya sekondari ROCHE, ambayo ipo umbali wa Kilometa 31 kaskazini mashariki mwa Halmashauri ya wilaya ya Rorya. Muhula wa kwanza wa masomo unaanza tarehe 11/01/2021. Unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe 11/01/2021 na mwisho wa kuripoti ni tarehe 19//01/2021 ndani ya siku saba.

2.0. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

2.1. SARE ZA SHULE

WASICHANA

Sketi mbili (2) aina ya cotton rangi nyeusi moja na kijivu moja.

- ✓ Marinda ya sketi yawe ya kati yasizidi kumi na mbili na yasipungue kumi Sketi zote zivuke goti, ziwe ndefu
- ✓ Mashati mawili (2) aina ya tetron/cotton meupe yenye mikono mifupi, yawe na kola na mifuko ya kushoto.
- ✓ Viatu vya ngozi vyeusi vya kamba jozi (2) na soksi nyeupe jozi (2) nyeupe
- ✓ Tai rangi nyeusi (1) na kijivu (1)
 - Sweta (1) rangi ya kijivu kwa ajili ya baridi.

WAVULANA

- ✓ Mashati mawili (2) aina ya tetron/cotton meupe yenye mikono mifupi na mifuko ya kushoto
- ✓ Suruali mbili (2), moja nyeusi na nyingine kijivu zenye mfuko kushoto, kulia na nyuma na ziwe na marinda matatu sio mshono wa modo.
- ✓ Tai nyeusi (1) na kijivu (1), urefu wa tai zote usivuke mkanda wa suruali. Mikanda (2) nyeusi isiwe na kichwa kikubwa au mapambo mengine
- ✓ Viatu vya ngozi vyeusi vya kamba jozi 2, soksi nyeusi jozi 2 Sweta rangi ya kijivu 1 kwa ajili ya baridi.

2.2 SARE ZA MICHEZO

WAVULANA: Bukta ya Bluu na Tisheti rangi ya Njano, njoo na viatu vya raba (zitavaliwa wakati wa kipindi cha michezo)

WASICHANA: Bukta au track (bluu) na tisheti ya rangi ya njano na viatu vya raba(zitavaliwa wakati wa kipindi cha michezo).

3.0. VIFAA VYA KUJIFUNZIA

Kalamu za wino 3, madaftari 10 (kaunta quire 3), penseli 2, rula 1 na mkebe wa hesabu(Mathematical set)